




Ndovu mmoja anaenda
kukunywa maji.



Twiga wawili wanaenda

kukunywa maji



Nyati watatu na ndege

wanne wanaenda kukunywa

maji pia.



Paa watano na ngiri

wanatembea wakielekea


kwenye maji.



Punda milia saba

wanakimbia wakielekea

kwenye maji.



Chura nane na Samaki tisa
wanaogelea kwenye maji.



Simba mmoja akaguruma.

Anataka kukunywa maji pia.

Ni nani anamwogopa

Simba?



Ndovu mmoja anakunywa
maji pamoja na Simba.